**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS – TAMISEMI**



**Shule ya Sekondari Ifakara,**

**S.L.P 148**

**IFAKARA.**

**Email: ifakarasec.edu@gmail.com**

**Tarehe 29/04/2025**

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ………….**
**S.L.P ……………………………………..**
**……………………………………………..**

Yah**: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI IFAKARA HALMASHAURI YA MJI IFAKARA MKOA WA MOROGORO MWAKA 2025.**

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka 2025 na atasoma tahasusi ya …………...
Shule ya Sekondari Ifakara ipo umbali wa Kilometa 2.5 Magharibi mwa Mji wa Ifakara Usafiri wa basi kutoka mjini Morogoro unapatikana katika kituo cha mabasi Msamvu/Mafiga Nauli ni Shilingi 15000/= hadi Ifakara stand ya Kibaoni, Toka Stand hadi shuleni Tumia Bajaji kwa shilingi 2000 kwa abiria.
Muhula wa Masomo unaanza tarehe 8/7/2025 hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe..................... Mwisho wa kuripoti ni tarehe ………………….
**MWANAFUNZI AJE NA NAKALA YA RESULT SLIP NA CHETI CHA KUZALIWA.**

**2. Mambo muhimu ya kuzingatia: -**
**2.1 SARE ZA SHULE:**

i. Sare ya shule ni sketi mbili ndefu mpaka chini, za rangi ya kijani kibichi kitambaa cha suti Kizito, mshono rinda box kwaajili ya darasani na sketi moja **ya KIJIVU** mshono huo huo kwaajili ya kushindia.(**ZINAPATIKANA SHULENI).**

ii. Mashati meupe ya mikono mirefu mawili aina ya tomato yasiyobana mwili. YENYE NEMBO yanapatikana shuleni

iii Rangi ya Hijab (kijuba) ni nyeupe kifunike kifua cha mwanafunzi pia iwe ndefu kufikia kifundo cha mkono akisimama kwa darasani na Hijab (kijuba) rangi ya dark blue kwa kushindia.

iv. Sare ya Michezo ni jezi rangi nyekundu.**zinapatikana shuleni.**

v. Viatu vya shule ni **raba nyeupe** isiyo na urembo yenye kamba isiwe na soli nene chini.

vi. Soksi jozi mbili au zaidi nyeupe za shule;

vii. sweta moja la kijani kibichi lenye ufito mweupe shingoni,mikononi na pindo ya chini LENYE NEMBO YA **SHULE linapatikana shuleni .**

viii. Tai moja ya kijani kibichi yenye mistari meupe **inapatikana shuleni**.

ix.Tisheti mbili zenye kola na NEMBO YA SHULE **zinapatikana shuleni.**

x. Raba nyeusi kwaajili ya michezo.

Xi. Aje na **tracksuit ya kijivu** zenye mistari meupe pembeni.

**NB: KUEPUKA KUCHANGANYA MISHONO NA RANGI,SARE ZENYE NEMBO YA SHULE ZINAPATIKANA SHULENI.**

**2.2 Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-**

i. Madaftari counter book qr 3 zisizopungua saba
ii. **Wanafunzi waje na Ream (A4)** ya Karatasi Mbili (2) kwa mwaka;moja kwa matumizi ya ofisi moja atahifadhi mwanafunzi kwa matumizi yake.
iii. Wanafunzi waliochaguliwa PCM waje na rim ya A3 MOJA na A4 moja asilete vifaa vya usafi vilivyoagizwa namba xii .
iv. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika vya mtaala mpya na kamusi kwa wanaosoma kiswahili na dictonary kwa wanaosoma kiingereza (english language).
v. Dissecting Kit kwa wanafunzi wanaosoma Biology na koti jeupe (lab coat) la maabara kwa wanafunzi wanaosoma masomo ya sayansi.
vi. Scientific Calculator FX 991 MS or ES
vii. Godoro kwa wanafunzi wa Bweni futi mbili na nusu. Aidha, godoro linaweza kukodishwa shuleni kwa gharama ya **Shilingi 10,000.00** kwa muhula kwa watakaowahi kwani ni machache.
viii. Mashuka Jozi 2 rangi ya light bluu, blanket 1, foronya ya godoro 1, chandarua 1 nyeupe ya pembe nne.
ix. Nguo za ndani za kutosha;
x. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe sio vya plastiki na sio containers;
xi. Ndoo 2 ndogo (lita Kumi) zenye mifuniko;

xii. Wanafunzi wote waje na vifaa hivi (***isipokuwa wanafunzi wa PCM na CBA***) ,Jembe lenye mpini 1,soft broom 1,hard broom 1,chelewa yenye mkono 1,toilet brush 1, ,dawa ya chooni arrow lita 2,squeezer 1.

*xiii.* Wanafunzi wanaosoma kilimo ( CBA) Waje na panga 1 na knapsack sprayer 1.*(pump ya kupulizia dawa/mbolea au maji kwenye mimea ya huvaliwa mgongoni)*

xiv. Wanafunzi wote waje na gum boot.

**xv. WANAFUNZI WENYE BIMA WAJE NAZO,GHARAMA ZA MATIBABU ZITAKUWA CHINI YA WAZAZI.( shule itaunganisha wenye uhitaji wa bima ya jamii iliyoboreshwa kwenye makundi ili waweze kulipa na kupatiwa)**



## 2.3 Michango mbalimbali

**a) Shule za Bweni**

| **Na** | **Aina ya Mchango** | **Kiasi** |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo ya vifaa vya shule | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha mwanafunzi | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

**LIPA KWENYE AKAUNTI NAMBA 21601100085 NMB,JINA LA AKAUNTI IFAKARA SECONDARY SCHOOL** ***mwanafunzi afike na bank pay in slip andika majina ya mwanafunzi.***

## 3. Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;

ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;

iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku( Preparation);

iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;

v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari;
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**

- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**

- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

**3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni
vii. Kufuga ndevu;
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xii. Kusababisha mimba;
xiii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiv. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xvi. Kudharau **Bendera** ya Taifa;
xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xviii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.
xix. Kugomea adhabu

**4. Viambatisho na Fomu Muhimu**



i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;
iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na
iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

5. **Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.**

**NB: MWANAFUNZI AFIKE SHULENI na Nakala (kopi) ya cheti cha kuzaliwa na nakala (kopi) ya cheti cha matokeo (result slips)**

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

**Saini ya Mkuu wa Shule ………………………………………**

**Jina la Mkuu wa Shule... Ngailo S**

**Mhuri wa Mkuu wa Shule ………………………………..**

**NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- **Mkuu wa shule .0752218504**
- **Makamu Mkuu wa Shule ...0717727579**
- **Mwandamizi Taaluma 0625926558**
  **sare za shule ...0625926558/0786004342/0789719419/0762222772/0786796588.**

**FORM NO 1**
**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**PRESIDENT OFFICE REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT**

**MEDICAL EXAMINATION FORM**

To be completed by a medical Office in respect of all Form Form V entrants
Student`s full name…………………………………………………………………………………….
Age/years………………………………Sex…………………………………………………………….…
Blood found (red and white) ………………………………………………………………………….
Stool examination……………………………………………………………………………………
Urinalysis……………………………………………………………………………………………..
Venereal Diseases test……………………………………………………………………………….
T.B Test……………………………………………………………………………………………….
Eye Test……………………………………………………………………………………………….
Ears…………………………………………………………………………………………………….
Chest…………………………………………………………………………………………………
Spleen………………………………………………………………………………………………….
Abdomen……………………………………………………………………………………………..
Urine for pregnant……………………………………………………………………………………

**ADDITIONAL INFORMATION (If any)**
eg Physical defects, impairment(s) eg arm, leg etc , infection chronic of family diseases etc
……………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………

I certify that, the above is fit to pursue further education as stated above

Signature…………………………………………..........................

Designation……………………………………………………………

**FOMU NA .2**
**SHULE YA SEKONDARI YA WASICHANA IFAKARA**

**TAARIFA ZA WANAFUNZI**

1.JINA LA MWANAFUNZI…………………………………………………………………..
2.KABILA……………………………………………………………………………………...
3.TAREHE YA KUZALIWA……………MWEZI………… MWAKA…………………………..
4.AMEZALIWA KATIKA WILAYA YA………………………MKOA WA………………………
5.DINI……………………………DHEHEBU……………………………………………………
6.JINA LA MZAZI……………………………………………………………………………
( ikiwa mzazi amefariki andika jina la mlezi hapa
7.ANUANI YA MZAZI/MLEZI
(KIJIJI)……………………………………………………………………….
(TARAFA)…………………………………………………………………….
(WILAYA)……………………………………………………………………
(MKOA)……………………………………………………………………….
Na. ya simu………………………………………………………….
8.KAZI YA BABA/MLEZI……………………………………………….…..
9.KAZI YA MAMA……………………………………………………………
10.Afya ya mwanafunzi (Kama ana ugonjwa unaohitaji uangalizi uandikwe. Taja udhaifu wowote wa
mwili au afya yake na uambatanishe cheti cha Daktari)

………………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………………
………………………………
11.Majina ya ndugu wengine wanaohusika na malezi ya huyu mwanafunzi (matatu tu), anuani zao kamili na Namba zao za simu
(a)Ndugu…………………………………………………. Uhusiano……………………………
(b)Ndugu………………………………………………. Uhusiano………………………………
(c)Ndugu………………………………………………. Uhusiano………………………………

**SAINI YA MWANAFUNZI ……………………………………**
**SAINI YA MZAZI/MLEZI………………………………………**

**FORM NO. 3**

**MKATABA/AHADI YA MWANAFUNZI**

Mimi………………………………………….. [jina kamili] ambaye ni mwanafunzi,nimeyasoma maagizo haya na kuyaelewa,ninakubali nafasi niliyopewa ya kujiunga na shule hii.

Ninaelewa wazi kwamba shuleni ni mahali pa kujifunza na mimi nina nia ya kujifunza.

Ninaelewa pia kuwa nafasi hii niliyopewa ni dhamana, hivyo naahidi mbele ya wazazi/walezi wangu ya kwamba nitaitumia vema nafasi hii kwa kushirikiana na uongozi wa shule kutimiza na na kutekeleza yale yote yaliyo katika maagizo haya ,nitatii na kufuata sharia za shule wakati wote.

Naahidi kutoshiriki katika migomo ,fujo, na makossa ya jinai .Naahidi pia kufanya bidii katika masomo yangu na kuwa mfano mwema kwa wenzangu wakati wote.

Saini ya mwanafunzi………………………………………………………………………………………

Tarehe……………………………………………………………………………………………

Shahidi…………………………………………………………………………………………….

Jina kamili………………………………………………………………………………………

Saini……………………………………………………………………………….……………

Tarehe…………………………………………………………………………….………………

**FORM NO.4**

**AHADI YA MZAZI;**

Mimi……………………………………………………………[jina kamili] ambaye ni mzazi/mlezi

Wa……………………………………………………...kidato cha……..Nimeyasoma maagizo haya na kuyaelewa vema.Nimekubali mwanangu ajiunge na shule hii.Naahidi kwamba nitashirikiana na uongozi wa shule katika kumpatia binti yangu malezi bora na nitatoa msaada kadri ya uwezo wangu nitakapotakiwa kufanya hivyo.Ninaahidi kwamba ninakubaliana na yote yaliyotajwa kwenye barua hii mfano sharia,kanuni, na maelekezo mengine yanayotolewa na shule.

Saini ya mzazi/Mlezi……………………………………………………………………….

Anuani kamili……………………………………………………………………………….

Simu………………………………………………………………………………………………….

Tarehe………………………………………………………………………………………………